# Sasisho za marufuku ya kusafiri

INTERNATIONAL RESCUE COMMITTEE

*Mwongozo huu ni kutikea Januari 5,2026*

**Marufuku ya kusafiri ni nini?**

Mnamo Juni 2025 Rais Trump aliamuru kuwa raia wa mataifa 19 wamepigwa marufuku kupokea visa kuingia Marekani. Mnamo Desemba 2025, aliongezea orodha ya mataifa ambayo raia wake wamepigwa marufuku kuingia Marekani. Kwa baadhi ya mataifa, Raia wote wamepigwa marufuku,na kwa Mataifa mengine,ni wale tu wanaoomba visa za kategoria fulani wamepigwa marufuku. Kuna hali za kipekee kwa wale walio na hali halali za kisheria hapa Marekani na wanaomba visa kwa sababu fulani. La muhimu, watu waliona visa halali zilizotolewa kabla ya 01/01/2026 wanaruhusiwa kuingia. Tazama habari zaidi kuhusu hali hizi za kipekee hapa chini.

**Ni Raia wa Mataifa gani wamepigwa marufuku kupata visa au kuingia Marekani chini ya marufuku ya kusafiri?**

| Marufuku ya visa kwa Raia wa Mataifa yafuatayo kwa wanaotafuta visa pamoja na wasiowahamiaji B-1,B2,B-1/B-2(Wageni),F(Wanafunzi), M(Mafunzo ya Ufundi), na J(kubalishana kitamaduni): | Marufuku ya visa kwa Raia wa Mataifa yafuatayo wanaotafuta visa za aina yoyote : |
|---|---|
| • Angola<br>• Antigua and Barbuda<br>• Benin<br>• Burundi<br>• Cote d'Ivoire<br>• Cuba<br>• Dominica<br>• Gabon<br>• The Gambia<br>• Malawi<br>• Mauritania<br>• Nigeria<br>• Senegal<br>• Tanzania<br>• Togo<br>• Tonga<br>• Turkmenistan<br>• Venezuela<br>• Zambia<br>• Zimbabwe | • Afghanistan<br>• Burkina Faso<br>• Burma<br>• Chad<br>• Republic of Congo (Brazzaville)<br>• Equatorial Guinea<br>• Eritrea<br>• Haiti<br>• Iran<br>• Laos<br>• Libya<br>• Niger<br>• Sierra Leone<br>• Somalia<br>• South Sudan<br>• Sudan<br>• Syria<br>• Yemen<br>• Watu waliona na hati za usafuri zilizotolewa na halmashauri ya Palestina |

**Kuna hali pekee kwa marufuku ya kusafiri?**

| Kategoria kadhaa za watu wanotafuta kuingia Marekani wameondolewa katika marufuku ya visa/kusafiri: | Pia, marufuku ya usafiri haiwahusu wafuatao: |
|---|---|
| • Raia wa Marekani<br>• Waakaji wa kudmu walio halali(LPRs, au wenye green card)<br>• Watu walio na uraia wa nchi mbili<br>• Baadhi ya watu wachache wa dini na kikabila kutoka Iran<br>• Baadhi ya wanadiplomasiana wanamichezo | • Yeyote alitetayari pata hali Marekani,wakiwemo wakimbizi, watafuta hifadhi, LPRs, na wale walio hapa kwa visa halali<br>• Yeyote aliye nje ya Marekani aliyekubaliwa,na ana visa halali au alipata visa kabla ya Januari 1,2026 |

**Je, na kama niko Marekani na ninaomba hali ya hifadhi au LPR/green card?**

Marufuku ya kusafiri haiwalengi watu walio Marekani wanaomba ruzuku za uhamiaji kama vile hifadhi au kuainisha hali( kubadilisha ) kuwa wakaaji wa kudumu. Walakini , USCIS imetia kikomo cha muda usindikaji wa maombi yote ya waomba hifadhi, na maombi ya kuainisha hali (green card) kwa wakimbizi wote na watu kutoka mataifa tajwa kwa marufuku ya kusafiri.

**Kama mimi ni mkimbizi,je mwenzi wangu wa ndoa/mtoto anaweza jiunga nami kupitia 1-730 mchakato wa jamaa mkimbizi/mwomba hifadhi?**

Marufuku ya usafiri haisemi kama wenzi wa ndoa na Watoto wa mkimbizi kutoka mataifa yaliyopigwa marufuku watapata kibali cha kuingia Marekani, lakini michakato ya wakimbizi wengi imesimamishwa chini ya makataa tofauti ya Serikali, kwa hivyo kuingia kama mkimbizi kutoka Mataifa mengi kwa sasa ni vigumu sana.

**Mimi ni mhifadhiwa, je mwenzi wangu wa ndoa/mtoto anaweza jiunga nami kupitia 1-730 mchakato wa jamaa mkimbizi/mwomba hifadhi?**

Marufuku ya usafiri haisemi kama mwenzi wa ndoa na Watoto wa mhifadhiwa walio pitishiwa ombi la uhifadhi kutoka Mataifa yaliyopigwa marufuku kuingia ataruhusiwa kuingia Marekani, lakini kuendelea kwa michakato inayosubiria kwa waomba hifadhi kutoka Mataifa yaliyopigwa marufuku imesimamaisha chini ya makataa tafauti ya Serikali. Watajwa kama waomba hifadhi kutoka Mataifa yasiyopigwa marufuku wana weza kuendelea na michakato ya kuingia Marekani.

**Je kama mimi ni raia wa Marekani au LPR(wenye green card), mwenzi wangu wa ndoa, mtoto au mzazi anaweza kuomba visa kujiunga nami Marekani kama wanatoka nchi mojawapo ya zilizopigwa marufuku?**

La. Chini ya amri ya Desemba ya marufuku ya kusafiri ,hamna hali za kipekee kwa jamii wa raia wa Marekani au LPRs.

**Je Waafghan wanaoomba visa maluumu za uhamiaji wanaondolewa katika marufuku ya kusafiri?**

La. Chini ya amri ya Desemba ya marufuku ya kusafiri, Waafghan wanaomba visa maluumu za uhamiaji hawataweza kupata visa tena.

**Niko na swali linalonihusu mimi au jamaa wangu aliye nje ya Marekani. Nina weza kupata usaidizi wapi?**

Kama bado hujafanya hivi,unapaswa kuwasiliana na mtoa huduma wa kisheria za uhamiaji. Unaweza kupata usaidizi hapa: https://www.immigrationadvocates.org/legaldirectory/or here: https://ailalawyer.com/